# TAARIFA YA KANUNI ZA FARAGHA

Idara ya Afya ya Jiji la Cincinnati

# TAARIFA YA KANUNI ZA FARAGHA
## IDARA YA AFYA YA CINCINNATI

## Maelezo Yako. Haki Zako. Majukumu Yetu.

Taarifa hii inaelezea jinsi taarifa za matibabu kukuhusu zinaweza kutumiwa na kufichuliwa na jinsi unavyoweza kupata taarifa hii. **Tafadhali ipitie kwa uangalifu.**

### Haki Zako

Una haki ya:

- Kupata nakala ya karatasi au ya kielektroniki ya rekodi yako ya matibabu
- Kusahihisha rekodi yako ya matibabu ya karatasi au ya kielektroniki
- Kuomba mawasiliano ya faragha
- Kutuomba tupunguze taarifa tunazoshiriki
- Kupata orodha ya wale ambao tumeshiriki nao taarifa yako
- Kupata nakala ya taarifa hii ya faragha
- Kuchagua mtu wa kukuwakilisha
- Kuwasilisha malalamiko ikiwa unaamini haki zako za faragha zimekiukwa

### Chaguo Zako

Una chaguo kadhaa kuhusiana na njia ambayo tunatumia na kushiriki taarifa wakati tunafanya yafuatayo:

- Kuambia familia na marafiki kuhusu hali yako
- Kutoa misaada ya maafa
- Kukujumuisha kwenye saraka ya hospitali
- Kutoa huduma ya afya ya akili
- Kutangaza huduma zetu na kuuza taarifa yako
- Kuchangisha fedha

### Matumizi na Ufichuzi Wetu

Tunaweza kutumia na kushiriki taarifa yako tunapofanya mambo haya:

- Kukutibu
- Kuendesha shirika letu
- Kutoza huduma zako
- Kusaidia kuhusiana na maswala ya afya na usalama wa umma
- Kufanya utafiti
- Kutii sheria
- Kujibu maombi ya mchango wa viungo na tishu
- Kushirikiana na mchunguzi wa matibabu au mwelekezi wa mazishi
- Kushughulikia fidia ya wafanyakazi, utekelezaji wa sheria na maombi mengine ya serikali
- Kujibu kesi za kisheria na hatua za kisheria

# Haki Zako

**Linapokuja suala la taarifa yako ya afya, una haki fulani.** Sehemu hii inaelezea haki zako na baadhi ya wajibu wetu katika kukusaidia.

#### Kupata nakala ya kielektroniki au karatasi ya rekodi yako ya matibabu

- Unaweza kuomba kuona au kupata nakala ya kielektroniki au karatasi ya rekodi yako ya matibabu na taarifa nyingine ya afya tuliyo nayo kukuhusu. Tuulize jinsi ya kufanya hivyo.
- Tutatoa nakala au muhtasari wa taarifa yako ya afya, kwa kawaida ndani ya siku 30 baada ya kupokea ombi lako. Tunaweza kutoza ada inayofaa, inayotegemea gharama.

#### Kuomba tusahihishe rekodi yako ya matibabu

- Unaweza kutuomba tusahihishe taarifa ya afya kukuhusu ambayo unafikiri sio sahihi au haijakamilika. Tuulize jinsi ya kufanya hivyo.
- Tunaweza kusema "hapana" kwa ombi lako, lakini tutakuambia sababu kwa maandishi ndani ya siku 60.

### Kuomba mawasiliano ya siri

- Unaweza kutuomba tuwasiliane nawe kwa njia mahususi (kwa mfano, kupitia simu ya nyumbani au ofisini) au kutuma barua kwa anwani tofauti.
- Tutasema "ndiyo" kwa maombi yote yanayofaa.

### Kutuomba tupunguze kile tunachotumia au kushiriki

- Unaweza kutuomba tusitumie au kushiriki taarifa fulani ya afya kwa ajili ya matibabu, malipo au shughuli zetu. Hatuhitajiki kukubaliana na ombi lako, na tunaweza kusema "hapana" ikiwa itaathiri huduma yako.
- Ukilipia mwenyewe huduma au bidhaa fulani ya huduma ya afya kikamilifu, unaweza kutuomba tusishiriki taarifa hiyo kwa madhumuni ya malipo au shughuli zetu kuhusiana na bima yako ya afya. Tutasema "ndiyo" isipokuwa sheria inatuhitaji tushiriki taarifa hiyo.

### Kupata orodha ya wale ambao tumeshiriki nao taarifa

- Unaweza kuomba orodha (kumbukumbu) ya nyakati ambazo tumeshiriki taarifa yako ya afya kwa miaka sita kabla ya tarehe unayoomba, ni nani tulishiriki naye, na sababu.
- Tutajumuisha ufichuzi wote isipokuwa ule kuhusu matibabu, malipo na shughuli za huduma za afya, na ufichuzi mwingine (kama vile wowote uliotuomba tufanye). Tutatoa rekodi moja kwa mwaka bila malipo lakini tutatoza ada inayofaa, inayotegemea gharama ikiwa utaomba kumbukumbu nyingine ndani ya miezi 12.

### Kupata nakala ya taarifa hii ya faragha

Unaweza kuomba nakala ya karatasi ya taarifa hii wakati wowote, hata kama umekubali kupokea taarifa hii kwa njia ya kielektroniki. Tutakupa nakala ya karatasi kwa upesi.

**Kuchagua mtu wa kukuwakilisha**

- Ikiwa umempa mtu fulani mamlaka ya uwakilishi wa matibabu au ikiwa mtu fulani ni mlezi wako wa kisheria, mtu huyo anaweza kutumia haki zako na kufanya chaguo kuhusu taarifa yako ya afya.
- Tutahakikisha kuwa mtu huyo ana mamlaka haya na anaweza kukuwakilisha kabla hatujachukua hatua yoyote.

**Kuwasilisha malalamiko ikiwa unahisi haki zako zimekiukwa**

- Unaweza kulalamika ikiwa unahisi tumekiuka haki zako kwa kuwasiliana nasi kwa kutumia maelezo yaliyo hapa chini.
- Unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Ofisi ya Haki za Kiraia ya Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani kwa kutuma barua kwa 200 Independence Avenue, S.W., Washington, DC 20201, kwa kupiga simu 1-877-696-6775, au kutembelea **www.hhs.gov/ocr/privacy/hipaa/complaints/.**
- Hatutalipiza kisasi kwa kuwasilisha malalamiko.

## Chaguo Zako

**Kwa taaifa fulani ya afya, unaweza kutuambia chaguo zako kuhusu kile tunachoshiriki.** Ikiwa una upendeleo wazi kuhusu jinsi tunavyoshiriki taarifa yako katika hali zilizoelezwa hapa chini, zungumza nasi. Tuambie unachotaka tufanye, na tutafuata maelekezo yako.

Katika hali hizi, una haki na chaguo la kutuambia tufanye mambo haya:

- Tushiriki taarifa na familia yako, marafiki wa karibu, au wengine wanaohusika katika huduma yako
- Tushiriki taarifa katika hali ya misaada ya maafa
- Tujumuishe taarifa yako katika saraka ya hospitali

*Ikiwa huwezi kutuambia upendeleo wako, kwa mfano ikiwa umepoteza fahamu, tunaweza kuendelea na kushiriki taarifa yako ikiwa tunaamini ni kwa faida yako. Tunaweza pia kushiriki taarifa yako inapohitajika ili kupunguza makali ya tishio kubwa na linalowezekana kwa afya au usalama.*

Katika hali hizi, hatuwezi kushiriki taarifa yako isipokuwa utupe ruhusa ya maandishi:

- Madhumuni ya utangazaji
- Uuzaji wa taarifa yako
- Kushiriki zaidi kwa rekodi ya

matibabu ya kisaikolojia Katika kisa cha

kuchangisha fedha:

- Tunaweza kuwasiliana nawe kwa juhudi za kuchangisha fedha, lakini unaweza kutuambia tusiwasiliane nawe tena.

# Matumizi na Ufichuzi Wetu

## Je, kwa kawaida tunatumiaje au kushiriki taarifa yako ya afya?

Kwa kawaida tunatumia au kushiriki taarifa yako ya afya kwa njia zifuatazo.

**Kukutibu**

Tunaweza kutumia taarifa yako ya afya na kuishiriki na wataalamu wengine wanaokutibu.

*Kwa mfano: Daktari anayekutibu jeraha anauliza daktari mwingine kuhusu hali yako ya afya kwa ujumla.*

**Kuendesha shirika letu**

Tunaweza kutumia na kushiriki taarifa yako ya afya ili kuendesha kituo chetu, kuboresha huduma yako, na kuwasiliana nawe inapohitajika.

*Kwa mfano: Tunatumia taarifa ya afya kukuhusu kudhibiti matibabu na huduma zako.*

**Kutoza huduma zako**

Tunaweza kutumia na kushiriki taarifa yako ya afya ili kutoza na kupata malipo kutoka kwa mipango ya afya au mashirika mengine.

*Kwa mfano: Tunatoa taarifa kukuhusu kwa mpango wako wa bima ya afya ili ilipie huduma zako.*

## Ni madhumuni gani mengine tunaweza kutumia au kushiriki taarifa yako ya afya?

Tunaruhusiwa au tunahitajika kushiriki taarifa yako kwa madhumuni mengine - kawaida kwa hali zinazochangia faida ya umma, kama vile afya ya umma na utafiti. Tunapaswa kukidhi masharti mengi katika sheria kabla ya kushiriki taarifa yako kwa madhumuni haya. Kwa maelezo zaidi angalia: www.hhs.gov/ocr/privacy/hipaa/understanding/consumers/index.html**.**

**Kusaidia kuhusiana na maswala ya afya na usalama wa umma**

Tunaweza kushiriki taarifa ya afya kukuhusu kwa hali fulani kama vile:

- Kuzuia magonjwa
- Kusaidia kuondoa bidhaa sokoni
- Kuripoti madhara mabaya ya dawa
- Kuripoti unyanyasaji, utelekezaji au vurugu ya nyumbani inayoshukiwa
- Kuzuia au kupunguza tishio kubwa kwa afya au usalama wa mtu yeyote

**Kufanya utafiti**

Tunaweza kutumia au kushiriki taarifa yako kwa ajili ya utafiti wa afya.

**Kutii sheria**

Tutashiriki taarifa kukuhusu ikiwa sheria za jimbo au shirikisho zinahitaji, ikiwa ni pamoja na Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ikiwa inataka kuona kwamba tunatii sheria ya faragha ya shirikisho.

**Kujibu maombi ya mchango wa viungo na tishu**

Tunaweza kushiriki taarifa ya afya kukuhusu na mashirika ya ununuzi wa viungo.

**Kushirikiana na mchunguzi wa matibabu au mwelekezi wa mazishi**

Tunaweza kushiriki taarifa ya afya na afisa mchunguzi wa vifo, mchunguzi wa matibabu, au mwelekezi wa mazishi wakati mtu anafariki.

**Kushughulikia fidia ya wafanyakazi, utekelezaji wa sheria na maombi mengine ya serikali**

Tunaweza kutumia au kushiriki taarifa ya afya kukuhusu:

- Kwa madai ya fidia ya wafanyakazi
- Kwa madhumuni ya utekelezaji wa sheria au na afisa wa utekelezaji sheria
- Na mashirika ya uangalizi wa afya kwa shughuli zinazoidhinishwa na sheria
- Kwa kazi maalum za serikali kama vile huduma za kijeshi, usalama wa kitaifa na ulinzi wa rais

**Kujibu kesi za kisheria na hatua za kisheria**

Tunaweza kushiriki taarifa ya afya kukuhusu ili kujibu amri ya mahakama au utawala, au kwa kujibu wito wa mahakama.

## Majukumu Yetu

- Usiri wa Rekodi za Mgonjwa wa Shida ya Matumizi ya Dawa za Kulevya - Hatutashiriki taarifa kutoka kwa rekodi za matibabu ya shida ya matumizi ya dawa za kulevya bila idhini yako ya maandishi au amri ya mahakama isipokuwa kama inavyoruhusiwa na sheria kwa matibabu ya dharura.
- Hali Zinazohusiana na VVU na UKIMWI - Hatutashiriki matokeo ya kipimo chochote cha VVU au Hali Inayohusiana na UKIMWI bila idhini yako ya maandishi au amri ya mahakama isipokuwa kama inavyotakiwa na sheria.
- Tunahitajika na sheria kudumisha faragha na usalama wa taarifa yako ya afya inayolindwa.
- Tutakujulisha mara moja ikiwa ukiukaji utatokea unaoweza kuwa umehatarisha faragha au usalama wa taarifa yako.
- Lazima tutii majukumu na mbinu za faragha zilizoelezewa katika taarifa hii na kukupa nakala yake.
- Hatutatumia au kushiriki taarifa yako isipokuwa kama ilivyoelezwa hapa isipokuwa utuambie tunaweza kuishiriki kwa maandishi. Ukituambia tunaweza kushiriki, unaweza kubadilisha mawazo yako wakati wowote. Tujulishe kwa maandishi ikiwa utabadilisha mawazo yako.

Kwa maelezo zaidi angalia: www.hhs.gov/ocr/privacy/hipaa/understanding/consumers/noticepp.html**.**

**Ikiwa una malalamiko kuhusu mbinu zetu za faragha au una maswali kuhusu taarifa hii, tafadhali wasiliana na Afisa wetu wa Faragha.**

Dr. Michelle Daniels
Cincinnati Health Department
3101 Burnet Avenue
Cincinnati, OH 45229
Namba ya simu (513) 357-7200
CHDprivacyofficer@cincinnati-oh.gov

## Mabadiliko ya Masharti ya Taarifa hii

Tunaweza kubadilisha masharti ya taarifa hii, na mabadiliko yatatumika kwa taarifa zote tulizo nazo kukuhusu. Taarifa mpya itapatikana ukiomba, ofisini mwetu na kwenye tovuti yetu.

Taarifa hii inaanza Kutumika tarehe 1 Juni 2022